# DARAJA YA AWALI YA SHULE YA UPILI

# KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

# GREDI 7 - 2024

***JS2402***

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

***JINA LA MWANAFUNZI :*** ____________________

***NAMBARI YA TATHMINI:*** ____________________

***TAREHE:*** ____________________

***JINA LA SHULE:*** ____________________

***MAAGIZO KWA MTAHINIWA***

1. Jibu maswali yote uliyopewa.
2. Umepewa kijitabu hiki cha maswali. Kijitabu hiki kina maswali 34.

***KWA MATUMIZI YA MTAHINI***

| | ZOEZI : 1 UFAHAMU WA KUSOMA (SWALI 1-12) Alama.17 | ZOEZI : 2 SARUFI (SWALI 13-24) Alama.21 | ZOEZI : 3 FASIHI (SWALI 25-28) Alama.12 |
|---|---|---|---|
| ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | |
| UPEO ( 50 ) | | | |
| KIWANGO CHA UTENDAJI | | | |

**Kijitabu hiki kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

© *compasspress, 2024*

**FUNGUA KURASA**



CamScanner

**ZOEZI LA 1: UFAHAMU**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 4***

Hapo zamani za kale katika tarafa ya Tulieni, palizuka kiangazi kikali, binadamu kwa wanyama walitaabika sana kwa kukosa lishe na maji. Wanyama walianza kupungua kutokana na vifo kwa kukosa chakula. Isitoshe, binadamu nao waliwawinda bila kujali maisha yao, ama kweli haki za wanyama zilikosa kuthaminiwa.

Baada ya muda mrefu wa kutaabika mfalme wa wanyama aliwaendea binadamu na kuwaeleza kuhusu haki zao. La kushangaza ni kuwa mfalme huyo alimweleza binadamu faida zao kwake. "Naam, sasa nimejua." binadamu alikubaliana na mfalme wa wanyama na kuapa kuwa angewalinda wanyama na kuwapa haki zao kwa vyovyote vile.

Binadamu aliapa kuwa mvua ikinyesha angepanda miti zaidi na nyasi ili wanyama wapate lishe na makao. Kweli mtu ni utu.

1. Taja wahusika wawili kwenye hadithi.**(alama 2)**

______________________________________________

______________________________________________

2. Taja haki zozote za wanyama zilizojitokeza kwenye hadithi. **(alama 1)**

______________________________________________

3. Binadamu alifanya nini ili kuwalinda wanyama? **(alama 1)**

______________________________________________

______________________________________________

4. Unadhani ni yapi yangetokea iwapo mfalme wa wanyama asingeongea na binadamu? **(alama 1)**

______________________________________________

______________________________________________



CamScanner

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu la 5 hadi la 8***

Wanyama wote waliumbwa na Mungu. Wanyama wana faida tele kwa binadamu. Hata hivyo, ni jambo la kushangaza kuona kuwa binadamu wawa hawa huwanyima wanyama haki zao hata baada ya kufaidika.

Wanyama kama mbwa humlinda binadamu, kuku humpa nyama na mayai, bila kumsahau ng'ombe ambaye hutupa maziwa. Binadamu hana budi kuwatunza wanyama na kuwapa uhuru wao.

Wanyama hawafai kubebeshwa mizigo mizito na kuchapwa, ni vyema kuwatunza vyema kwa kuwapa chakula cha kutosha, kuwapa dawa wakiwa wagonjwa na kuyatunza mazingira yao. Hatufai kuikata miti ovyo, ndege na wanyamapori huishi mbugani, tusipoyalinda mazingira, tutakuwa tukiwaangamiza wanyama na hatutapata faida zinazotokana na wanyama hao. Je, wewe unaweza kufanya nini ili kuendeleza uhuru wa wanyama?

5. Kifungu hiki kinazungumzia nini? **(alama 1)**

________________________________________

________________________________________

6. Ni mambo gani matatu yanayoonyesha uhuru wa wanyama? **(alama 3)**

________________________________________

________________________________________

________________________________________

7. Taja faida yoyote tunayopata kutokana na wanyama. **(alama 1)**

________________________________________

________________________________________

8. Je, unaweza kufanya nini ili kuendeleza uhuru wa wanyama? **(alama 2)**

________________________________________

________________________________________



CS CamScanner

***Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la 9 hadi la 12***

Damu ni nzito kuliko maji. Maana ya methali hii ilikuwa wazi kwa Tausi baada ya mtoto wake kuugua. Tausi alikuwa katika matatizo yaliyokithiri baada ya kukosa kazi kwa muda mrefu. Si kwamba hakutafuta kazi bali alikaa nyumbani akimtunza mwanawe. Alitumia akiba yake ikaisha na bado mwana wake alihitaji lishe bora.

Alimwendea dada yake na kumwomba ampige jeki kwa fedha. Dada yake hakupinga bali aliamua kumsaidia. Walimpeleka mtoto wao hospitalini ambapo alitibiwa. Aidha, walishauriwa kila mara kando na kumpa dawa, wawe wakizingatia kumpa lishe bora ili afya yake iimarike na ajikinge dhidi ya maradhi. Ama kweli, kinga ni bora kuliko tiba.

**9.** Taja methali mbili zilizotumika kwenye kifungu. **(alama 2)**

_______________________________________________

_______________________________________________

**10.** Kwa nini Tausi alihitaji kusaidiwa? **(alama 1)**

_______________________________________________

_______________________________________________

**11.** Iwapo unaugua, unapaswa kufanya nini kulingana na kifungu? **(alama 1)**

_______________________________________________

**12.** Je, afya zetu zitaimarika tukifanya nini? **(alama 1)**

_______________________________________________



CamScanner

**ZOEZI 2: SARUFI**

***Soma kifungu kifuatacho kina nafasi 13 mpaka 17. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.***

Usafi ___**13**___ kibinafsi unafaa kutiliwa maanani na kila mmoja. Ni vyema kupiga meno mswaki, kuoga na kukaa kwenye mazingira ___**14**___. Uchafu hutuletea magonjwa ___**15**___ hutuathiri ___**16**___ shughuli ___**17**___ za kila siku.

**13.** A. ya B. wa C. na D. za

**14.** A. safi B. usafi C. uchafu D. chafu

**15.** A. ambao B. ambazo C. ambayo D. ambalo

**16.** A. kwa B. na C. badala ya D. katika

**17.** A. zetu B. yetu C. kwetu D. letu

**18.** Pigia mstari maneno yenye sauti **'dh'** na **'th'** kwenye sentensi. **(alama 1)**

**Mwanadamu anayethamini amani alimpa dhamani.**

**19.** Akifisha sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

**Ufupisho wa sanduku la posta ni**

______________________________________________________



CamScanner

**Kamilisha nomino za makundi kwa kutumia majibu uliyopewa kwenye mabano. (alama 4)**

**(kicha, mkungu, bunda, umati)**

20. ________________ wa watu ulizingatia lishe bora.

21. Nitatumia ________________ la noti kununua mboga na matunda.

22. Kabla ya kuwauzia wateja ________________ cha mboga ni vyema kuziosha.

23. Tuliwapelekea ________________ wa ndizi jana.

24. Chagua nomino dhahania kutoka kwenye kadi ifuatayo. **(alama 2)**

| **Mashuke, Wema, Mlima, Furaha, Nakuru, Maji, Uteo, Upole, Chuki** |
|---|

________________________________________

25. Pigia mstari nomino za wingi kwenye sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

**Maji safi yalipewa ng'ombe wa maziwa na kaka.**

26. Taja matumizi ya kikomo na uandike mfano wa sentensi. **(alama 3)**

________________________________________

________________________________________

________________________________________

27. Taja vipengele viwili vya kuzingatia katika kujibu mazungumzo. **(alama 2)**

________________________________________

________________________________________



CamScanner

## ZOEZI LA 3:FASIHI

28. Andika sifa mbili za fasihi andishi.**(alama 2)**

29. Taja sifa mbili za fasihi simulizi.**(alama 2)**

30. Andika maana ya nyimbo za watoto na sifa zake mbili. **(alama 4)**

31. Andika maana ya bembelezi na sifa zake mbili. **(alama 4)**



CamScanner

**Andika insha ya kubuni kuhusu:**

## SAFARI YA KUPENDEZA



CamScanner